

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

BARUA ZOTE ZIPELEKWE KWA MKURUGENZI WA JIJI

SIMU: 2123551/5
NUKUSHI: 2125589
BARUA PEPE: cd@dcc.go.tz



P.O. BOX: 9084
UKUMBI WA JIJI
1 BARABARA YA MOROGORO
11882 DAR ES SALAAM
TANZANIA

Tarehe: 10/04/2019

YAH: TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MBIO ZA DAR 10 K RUN ZITAKAYOFANYIKA SIKU YA MEI MOSI JIJINI DAR ES SALAAM

Ni fahari kwetu Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuwepo mahala hapa, na hasa kuonesha ushirikiano wetu pamoja na wadau mbalimbali, hususani katika sekta ya michezo na utalii.

A. Shukrani za kipekee tunapeleka kwa Kampuni ya Eye Promoter chini ya ndugu Manase;

- **Kwanza**, kwa kuandaa 'Dar Ten 10 K Run', tukiwa na imani kwamba tukio hili litawaleta pamoja wana Dar es Salaam, Watanzania na watu kutoka Mataifa mbalimbali katika Jiji letu. Tunawahamasisha na kuwakaribisha wote kushiriki mbio hizi za Dar Ten K na kufurahia uwepo wao ndani ya Jiji letu.
- **Pili**, Kwa kuiunga mkono Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuandaa tukio linalohamasisha **amani** kati yetu; kwani Dar 10 K itashirikisha watu wengi na tofauti, sote tutakutana na kushiriki kwa pamoja kwa amani na upendo. Pia tukio hili ni fursa muhimu kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuhamasisha mazoea ya kupenda kufanya mazoezi kwa ajili ya kulinda afya zetu, kuhamasisha michezo na utalii katika Jiji letu la Dar es Salaam.
- **Tatu**, kwa kuona umuhimu wa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kama sehemu ya 'Taasisi wadau' ambao ni muhimu katika kufanikisha tukio hili la Dar 10 K na hasa kwa kuzingatia kwamba Halmashauri ya Jiji kwa sasa inachukua hatua kubwa katika kuhamasisha sekta ya utalii Jijini, **'Dar City Tour'**.
- **Nne**, tunatoa shukrani za dhati kwa Eye Promoter kwa kuchagua kufanya Press Conference hii ndani ya Jengo letu la kitalii la Old Boma ikiwa ni pamoja na kujumuisha picha ya jengo la Old Boma katika Medali za Dar 10 K 2019; hii ni heshima kubwa na fursa kwa watu wote kutambua uwepo wa jengo hili la kale zaidi jijini Dar es Salaam likijengwa mnamo mwaka 1866 na Sultan Majid wa Zanzibar.

Jengo hili linalomilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na kuendeshwa kwa ushirikiano na Kituo cha ubunifu wa Majengo Dar es Salaam (Dar es Salaam Center for Architectural Heritage 'DARCH') ni sehemu ya Urithi wa Majengo jijini na liko wazi kwa wote kufika na kujionea sehemu ya maonesho ya historia ya Jiji, duka la vifaa vya

asili pamoja na mgahawa mzuri ulioko sehemu ya juu ya jengo (Rooftop restaurant).

B. Ofisi za Utalii, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam zinapatikana ndani ya jengo hili la Old Boma. Ofisi yetu kwa namna ya kipekee inaandaa aina mbalimbali za safari za kitalii jijini na maeneo jirani ya utalii:

- **Dar City Tour:** Mahsusi kuwatembeza watalii wa ndani na nje kuweza kufurahia utalii wa historia ya Jiji, bionuai (Biodiversity), utamaduni, fukwe na mandhari ya Jiji.
- **Kigamboni Tour**
- **Visiwa vya Mbudya, Bongoyo na Sinda**
- **Bagamoyo tour**
- **Saadani, Mikumi, Selous na vivutio vingine vinavyopakana na Jiji la Dsm.**

C. Basi la Utalii: Kwa sasa Halmashauri ya Jiji ina miliki basi la kitalii mahsusi kwa makundi ya watalii, wanafunzi, na makundi mbalimbali ya wafanyakazi, vikundi vya kijamii kuweza kushiriki katika utalii huu.

D. Bajaji za Utalii: Kwa sasa pia Halmashauri ya Jiji ina bajaj nzuri zinazotumika kubeba wageni lakini pia kutolea taarifa za utalii wa Jiji na nchi kwa ujumla (Mobile Tourist Information)

MWISHO: Kwa fursa hii, napenda kuwahamasisha watu wote wakiwemo wafanyakazi wa Halmashauri ya Jiji na Manispaa zote za Dar es Salaam kuwahi mapema kujiandikisha kwa ajili ya Dar 10 K Run na kwa umuhimu mkubwa nawahamasisha Watanzania kupenda Utalii wa ndani na hasa Utalii na vivutio vya Utalii vilivyopo Jijini Dar es Salaam, Halmashauri ya Jiji imejizatiti kuhamasisha na kutoa huduma hii ya Utalii kwa viwango vikubwa ili kuweza kulimudu soko la ndani na nje.


Gaston Makwembe

**K.n.y: MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM.**